# CAG aanika udhaifu wa usafiri wa umma mijini

Juma Isslahaka, Mwananchi
jissihaka@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Usafiri wa umma mijini nchini Tanzania unakabiliwa na majanga, baada ya magari ya huduma za jamii kupungua kwa asilimia 55, huku daladala zikipungua kwa asilimia 19, hali inayochangiwa na uratibu usioridhisha wa mamlaka husika.

Ukistaajabu kuporomoka kwa njia hizo za usafiri wa umma, utekelezaji wa malengo ya Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Dar es Salaam utakushangaza, kwani umeshuka hadi asilimia sifuri, kutokana na kudorora kwa uwekezaji na msaada wa kitaasisi.

Hayo ni kwa mujibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, kupitia ripoti yake ya ukaguzi wa ufanisi ya mwaka wa fedha unaoanzia Julai 2024 hadi Juni 2025. Tathmini ikifanywa katika majiji ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Mbeya.

Ripoti hiyo, inaweka wazi kuwa hali hiyo inasababishwa na udhaifu katika upangaji na uratibu wa mamlaka zinazohusika na usafiri na kukosekana kwa mikakati madhubuti ya usafiri mijini itakayowezesha uhimilivu na uboreshaji wa huduma rasmi za umma.

"Huduma za usafiri wa mijini katika majiji makubwa, nilibaini kuwa uhakika wa huduma hizo uliathiriwa na kuenea kwa shughuli zisizo rasmi ambazo hazikuwa na ratiba maalumu wala viwango vya huduma vinavyodhibitiwa," anasema kupitia ripoti hiyo.

Kwa sababu hiyo, anasema watumiaji wa usafiri huo mara nyingi walikumbana na muda wa kusubiri usiotabirika na hali mbaya ya vyombo vya usafiri.

## Utoaji leseni tatizo

Katika ripoti hiyo iliyowasilishwa bungeni jana, CAG anasema alibaini mfumo wa utoaji leseni na udhibiti wa watoa huduma unavutia watoa huduma wasio rasmi wa usafiri wa mijini.

Aidha, anasema alibaini Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (Latra), imekuwa ikitoa leseni kwa watoa huduma za usafiri wa mijini wanaotumia vyombo vyenye uwezo mdogo wa kubeba, abiria zikiwamo bajaji na pikipiki kinyume na Aya 5.7.2.2 ya Sera ya Taifa ya Usafirishaji ya mwaka 2003.

Aya hiyo, anasema inahimiza usafiri wa umma wa watu wengi kwa kutilia mkazo uingizaji na utoaji wa leseni kwa magari ya abiria yenye uwezo wa kubeba abiria kuanzia 30 kwa mabasi madogo hadi 90 kwa mabasi makubwa.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, uchambuzi wa taarifa za leseni za usafirishaji kwa robo ya nne, ukijumuisha miaka ya fedha 2020/21 hadi 2024/25 ulionyesha usafiri wa umma wa watu wengi haukusajiliwa wala kupewa leseni.

"Hata hivyo, Latra imekuwa ikitoa leseni kwa watoa huduma za usafiri wa umma wenye vyombo vyenye uwezo mdogo, jambo lililosababisha ongezeko la asilimia 95 kufikia mwaka wa fedha 2024/25," naeleza ripoti hiyo.

Inakwenda mbali zaidi na kubainisha, kati ya mwaka wa fedha 2020/21 na 2024/25, usajili wa pikipiki uliongezeka kwa asilimia 145 kutoka 18,408 hadi 45,078, na kuzifanya kuwa aina ya usafiri wa mijini uliopewa leseni zaidi.

## Kupungua daladala, mwendokasi

Ripoti hiyo inaeleza, kwa kupungua magari ya huduma za jamii kwa asilimia 55 na daladala kwa asilimia 19, huduma za usafiri wa mabasi yaendayo haraka ilishuka hadi asilimia sifuri, ikiashiria uwekezaji mdogo na usaidizi usioridhisha wa kitaasisi.

"Nilibaini kuwa hali hii ilitokana na upangaji na uratibu usiojitosheleza miongoni mwa Latra na kukosekana kwa mikakati jumuishi ya usafiri wa mijini ili kuwezesha uhimizaji na uboreshaji huduma rasmi za umma," imeeleza ripoti hiyo.

Matokeo yake, ripoti inaeleza miji mikubwa inakabiliwa na hali mbaya ya mchanganyiko wa magari barabarani, inayosababisha msongamano, muda mrefu wa kusafiri na ongezeko la ajali za barabarani, mambo ambayo huwa yanaathiri upatikanaji wa usafiri bora na salama mijini.

"Mapitio yangu ya utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Usafiri 2020/21 hadi 2024/25 katika majiji ya Dar es Salaam, Mbeya, Arusha, na Mwanza yalibaini ucheleweshaji wa mara kwa mara, usimamizi usioridhisha, ukosefu wa utengamano na utekelezaji usioridhisha wa hatua zilizopangwa.

"Juhudi muhimu, ikiwemo upanuzi wa miundombinu ya usafiri wa mabasi yaendayo haraka katika Jiji la Dar es Salaam, kuwapo kwa njia maalumu za usafiri wa umma, kuwapo kwa vituo vikuu vya usafiri vinavyounganisha njia mbalimbali, mipango ya kupunguza msongamano na uunganishaji wa mfumo wa barabara na vivuko, hazikutekelezwa kikamilifu," imesema.

> **"Watu wanautumia vibaya uhuru wa kutoza nauli kwenye bodaboda na bajaji. Wengi wanatoa huduma kama daladala na hata baadhi ya wamiliki wa daladala wanauza wananunua bodaboda na bajaji."**
>
> Dk Habib Saluo

Hali hiyo, anasema ni kinyume na matakwa ya aya ya 2.3 na 2.4 ya Sera ya Taifa ya Usafirishaji ya mwaka 2003, inayotaka mipango kabambe ya usafiri wa mijini iwiane na mikakati ya kitaifa ya usafiri ili kuhakikisha mifumo jumuishi, yenye ufanisi na endelevu.

Upungufu huo pia, Kichere anasema unajumuisha miradi ambayo haijatekelezwa kama njia maalumu za usafiri wa umma, muunganisho wa mifumo ya usafiri na ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi iliyopangwa.

Anatolea mfano kuunganisha barabara na kivuko jijini Mwanza na utekelezaji wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka awamu ya pili jijini Dar es Salaam.

## Chanzo cha foleni

Upungufu huo, CAG anasema ulitokana na kutotafsiriwa ipasavyo kwa Sera ya Taifa ya Uchukuzi ya mwaka 2003 na mipango ya Taifa ya usafiri kuwa mipango inayotekelezeka katika ngazi ya miji na kutoingizwa kwa vipaumbele katika hatua za mipango mikuu.

"Kukosekana kwa uwiano huo kulisababisha msongamano wa kudumu, upatikanaji mdogo na kuongezeka kwa huduma zisizo rasmi za usafiri," anasema.

## Huduma na idadi ya watu

Katika ripoti hiyo, CAG Kichere anasema alibaini huduma za usafiri katika miji hiyo hazikidhi mahitaji ya idadi ya watu inayoongezeka, huku kukiwa na changamoto katika upatikanaji wa usafiri wa uhakika na gharama nafuu.

Pia, amebaini miundombinu ya usafiri iliyopo haikusaidia ukuaji


### AHUENI >

## Uwekezaji mpya

Licha ya ukaguzi uliofanyika hadi Juni 30, 2025, Januari mwaka huu mabasi 49 kati ya 99 yaliyonunuliwa na Serikali kwa ajili ya kutoa huduma katika awamu ya kwanza ya mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT), yaliwasili nchini.

Kwa mujibu wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Profesa Rizik Shemdoe, Serikali ilitoa Sh20 bilioni, kwa ajili ya ununuzi wa mabasi hayo.

Vile vile, Agosti mwaka jana, Kampuni ya Mofat Limited, iliingiza mabasi 99 yaendayo haraka na tayari yameanza kutoa huduma katika njia ya Gerezani-Mbagala. Idadi hiyo ya mabasi ni kati ya yale 250, yaliyopangwa kununuliwa na kampuni hiyo.




Chanzo: Ripoti ya mwaka ya CAG 2024/2025

MwananchiData